JINA: _____

NA: _____

MAAGIZO YA KUJIUNGA NA MAFUNZO YA UALIMU

1. **ASTASHAHADA YA UALIMU ELIMU YA MSINGI-Miaka miwili**
2. **ASTASHAHADA YA UALIMU ELIMU YA AWALI-Miaka Miwili**

UTANGULIZI

Tunafurahi kukutaarifu kuwa umechaguliwa kujiunga na Mafunzo ya Astashahada ya Ualimu Elimu ya Msingi/Awali kwa mwaka wa masomo 2018/2019. Hii ni nafasi ya pekee kwako kwani wengi hawakubahatika kuipata. Ni matumaini yetu kwamba ufikapo hapa Chuoni utaitumia fursa hii vizuri.

Chuo cha Ualimu Mhonda kipo katika Mkoa wa Morogoro, Wilaya ya Mvomero, Tarafa ya Turiani, kata ya Mhonda, kijiji cha Mhonda. Ni umbali wa kilometa 104 kutoka Morogoro mjini, na kilometa 3 ½. kutoka Turiani-Mapate/Soko la ndizi hadi Chuoni.

NAMNA YA KUFIKA CHUONI

i) Ufikapo kituo cha **Mabasi** Morogoro (Msamvu), Panda basi linaloelekea Turiani mojawapo ni; BM COACH, ZENJIBAR, KVC, MSUYA, ZEELAND, AU NOAH. Nauli yake ni kati ya Tsh. 5000/= hadi 5500/= tu.

ii) Ufikapo Turiani shuka katika kituo cha Mapate/Soko la Ndizi, chukua usafiri kuelekea Chuoni nauli ya pikipiki ni Tsh 1500/= hadi 2000/= tu aidha zipo NOAH za kukodi kwa gharama ya Tsh. 10,000/=. **NB:** Unashauriwa kufika Chuoni mapema kabla ya saa 12.00 jioni.

A: KUSAJILIWA CHUONI

Mara ufikapo Chuoni pitia hatua zifuatazo ili kukamilisha usajili wako:

i) Onana na mlinzi ili upate maelekezo

ii) Onana na Msajili wa Wanachuo ili uwasilishe, vyeti halisi/Result slip na nakala zake. Vyeti hivyo ni

(a) Cheti cha kidato cha nne (Form four Academic Certificate/ Result slip)

(b) Cheti cha kidato cha sita (Form six Academic Certificate/Result slip kwa aliyehitimu)

(c) Vyeti vya kuhitimu Shule (School Leaving Certificates- kama unacho)

(d) Cheti cha kuzaliwa

(e) Cheti cha ndoa (Kwa aliyeoa/aliyeolewa)

(iii) Onana na Mhasibu/Msarifu wa Chuo ili ukabidhi risiti za Ada na Michango uliyolipia Benki.

(iv) Onana na Boharia ili kukabidhi vifaa

(v) Onana na Mratibu Taaluma ili upangiwe darasa.

(vi) Onana na Mwadili wa wanachuo ili upangiwe bweni

NB: Chuo hakitampokea na kumsajili Mwanachuo:

a) Atakayekuja bila vyeti halisi (originals) hatapokelewa. Aidha, kwa yeyote atayewasilisha vyeti visivyo halali hatua zitachukuliwa dhidi yake ikiwa ni pamoja na kupelekwa Polisi.

b) Kama hutakamilisha malipo ya Ada na Michango yote hautapokelewa. Aidha, kwa wale wanaofadhiliwa na mashirika waje na vithibitisho vyao vyenye saini na muhuri wa shirika/idara husika.

B: MAHITAJI MUHIMU KWA WANACHUO

i) **SARE**;Wanaume na wanawake waje na mashati **2** ya mikono mirefu ya bluubahari na tai ndefu nyeusi. Mashati yawe marefu ili uweze kuchomekea vizuri yanapovaliwa. (ii) Wanaume waje na Suruali nyeusi 2 zenye marinda (cerebration) na mifuko mitatu na mkanda mweusi wenye Bakozi ya saizi ya kati. (iii) Wasichana washone sketi 2 nyeusi kwa kutumia kitambaa cha suti, ziwe sketi za linda box mbele tu na ndefu za kuvuka magoti . **Watakaotumia hijabu washone sketi nyeusi, shati/nusu kanzu na juba (vyote viwe vya bluubahari)**. (iv) Koti la suti nyeusi linaloendana na suruali au sketi. v) Unatakiwa kuwa na mavazi machache yenye heshima na hadhi yatakayotumika baada ya vipindi vya darasani.

NB: Nguo za kubana, fupi, zinazoangaza, mipasuo kupita kiasi, pensi nyanya, timberland na nyingine za aina hiyo haziruhusiwi Chuoni. Unatakiwa kuja na begi dogo la kuhifadhia vifaa na nguo zako.

(vi) Uwe na viatu vyeusi vya ngozi vyenye visigino vifupi vya kutumbukiza kwa jinsi zote (Me/Ke). Soksi jozi 2 au zaidi nyeupe kwa wasichana na nyeusi kwa wavulana. (vii) Nguo za michezo: (a) Bukta za blue kwa wanaume na Sketi za solo rangi ya darkblue kwa wanawake **uje nayo.** (b) Tracksuit zenye michirizi mweupe (Wanaume iwe ya kijani na wanawake iwe ya nyekundu) **uje nayo.**

(viii) Shuka nne au zaidi moja iwe nyeupe isiyo na marembo yoyote, mto na foronya nyeupe, Chandarua cheupe cha pembe nne

chenye ukubwa wa nne kwa sita (4x6) kwani eneo hili lina mbu wengi.

(ix) File folder 2 kwa ajili ya kuwekea kumbukumbu binafsi na **Rimu mbili (2) za Karatasi za A4, moja ya chuo** na nyingine kwa matumizi yako binafsi.

(x)) Mathematical set, daftari kubwa 14 za kuanzia, rula ya futi moja, Kalamu na penseli za kutosha.

(xi) Vifaa vya chakula viwe vya bati au mfupa mgumu, ambavyo ni sahani, bakuli, kikombe, na kijiko (**vyombo vya plastiki haviruhusiwi).** Galoni la kuhifadhia maji ya kunywa na ndoo kubwa ya kuogea. (xii) **Wasichana** waje na jembe lenye mpini na soft brush na kwa **Wavulana** waje na kwanja na soft brush moja.

(xiii) Vifaa vingine: tochi na mwamvuli kwa matumizi yako binafsi. **NB:** Vyombo vya chakula, ndoo ya kuogea, daftari, kalamu, Rimu ya karatas, jembe, kwanja na softbrush vinauzwa katika duka lililopo chuoni. Aidha, unatakiwa kuwa na fedha za kutosha kwa ajili ya matumizi yako binafsi.

C: ULIPAJI WA ADA NA MICHANGO

Unapofika Chuoni utatakiwa kutoa risiti mbili za malipo ya ada na Michango kama ilivyofafanuliwa hapa chini;

AINA YA MCHANGO	**KIASI KWA**	
	Muhula	**Mwaka**
Ada ya Mafunzo	300,000/=	600,000/=
Mtihani wa Taifa kwa Mafunzo	50,000/=	50,000/=
Huduma ya kwanza	5,000/=	5,000/=
T-shirts 2 kwa	30,000/=	30,000/=
Mafunzo		
Serikali ya wanachuo	2,500/=	5,000/=
Tehama/ ICT	10,000/=	20,000/=
Elimu kwa Michezo	5,000/=	10,000/=
Kukodisha godoro	10,000/=	20,000/=
Usafi na Miundombinu	10,000/=	20,000/=
Usajili	5,000/=	5,000/=
Taaluma	25,000/=	50,000/=
Kitambulisho Muda wote wa Mafunzo	5,000/=	5,000/=
Tahadhari	10,000/=	20,000/=
Ulinzi	7,500/=	15,000/=
Mahafali kwa mwaka	5,000/=	5,000/=
Bima ya Afya **asiyekuwa nayo**	50,400/=	50,400/=
JUMLA	**530,400/=**	**910,400/=**

N.B: Pesa taslimu **haipokelewi** chuoni.

(i) **ADA** yote **Tsh 300,000 kwa Muhula au Tsh 600,000 kwa Mwaka** ilipwe katika benki ya **NMB** kwenye akaunti namba **22010000456** jina la akaunti ni **UCHANGIAJI ADA ZA CHUO MHONDA**.

(ii) **MICHANGO** yote ilipwe katika benki ya **NMB** kwenye akaunti namba **22001100005** jina la akaunti ni **MHONDA T.C.**

Aidha, fedha aa matumizi binafsi ya mwanachuo **zisiwekwe** kwenye akaunti hizo hapo juu kwani akaunti za serikali haziruhusiwi kuweka au kutoa fedha za matumizi binafsi ni vema mwanachuo akafungua akaunti yake binafsi.

D: UTHIBITISHO WA AFYA

Unapaswa kupimwa afya yako kabla ya kufika Chuoni na daktari yeyote wa Hospitali inayotambulika Serikali. Iwapo utakuja bila uthibitisho wa daktari udhuru wowote hautapokelewa. Kama unatumia dawa maalum kulingana na maradhi yako uje na dawa zako. Chuo kinatoa matibabu ya huduma ya kwanza tu. Fomu ya kupimwa afya yako inapatikana kwenye website ya chuo. NB: Aidha matibabu yoyote ya mwanachuo yanafanywa na mzazi/mlezi hivyo mwanachuo mwenye **kadi ya Bima ya afya** anashauriwa aje nayo.

E: CHAKULA

Chuo kinatoa Chakula lakini hakitoi chakula maalumu (special diet) kwa Mwanachuo yeyote.

F: SHUGHULI ZA NJE.

(i) Uzalishaji Mali

Katika jitihada za kuendeleza Elimu ya kujitegemea, Chuo kina miradi mbalimbali inayoendeshwa na Wanachuo wenyewe. Kila Mwanachuo atapaswa kushiriki kikamilifu katika shughuli za uzalishaji na ujenzi wa Taifa.

ii) Utunzaji wa Mazingira na Mali za Chuo

Ufikapo Chuoni utagawiwa eneo la kutunza.

Ni matarajio yetu kwamba utatunza Majengo na Mazingira ya Chuo kulingana na maelekezo utakayopewa. Utawajibika kutunza mali ya umma utakayokabidhiwa na Chuo na ya kwako binafsi. Ukipoteza au kuharibu mali hiyo utalazimika kulipa.

G: SHERIA ZA CHUO

Utapaswa kufuata sheria, kanuni na taratibu zote za chuo kwa muda wote wa mafunzo, sheria hizo utazikuta hapa chuoni.

J: KUFUNGUA CHUO

i. Chuo kitafunguliwa rasmi tarehe **04/10/2018**.
ii. Masomo yataanza rasmi tarehe **08/10/2018**
hakikisha unaingia darasani kwa tarehe hiyo bila kukosa.

MOTO WA CHUO: **ELIMU ILETE USAWA WA BINADAMU.**

DIRA YA CHUO: **“Kuandaa Walimu Walio Bora, Wazalendo, Wenye Maadili, Wanaojali Jinsia, Haki na Wajibu, Kwa Kutumia Miundo Mbinu Thabiti Kwa Kuzingatia Mahitaji ya Jamii na Taifa**

WITO WA CHUO: **“Chuo kuwa Chachu ya Mabadiliko Chanya Kitaaluma, Kitaalam na Kimaadili kwa Kuchochoea Ubunifu, Udadisi, Utafiti na Kuthubutu Kutenda ili Kuiwezesha Jamii Kukabiliana na Changamoto Zitokanazo na Mabadiliko ya Sayansi na Teknolojia katika Kuleta Mabadiliko Endelevu Ifikapo 2022”**

JUMUIYA YA CHUO INAKUKARIBISHA CHUONI MHONDA WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA

CHUO CHA UALIMU MHONDA

KARIBU SANA

CHUO CHA UALIMU MHONDA

S.L.P. 14, TURIANI

Email: mhondatc@gmail.com
Website: www. mhondatc.weebly.com



.....
G. L. MNYANYI
MKUU WA CHUO

MAWASILIANO

Tumia namba za simu zifuatazo:

UTAWALA

+255784381147/+255713468781/+255763815205

USAJILI

+255714910720/+255784595836/+255763589385

TAALUMA

+255752880668/+255757864504+255685134230

UADILI

+255754889193/ +255714261895